# الذَّكَاةُ

# شُرُوْطُهَا وَآدَابُهَا

# KUCHINJA

## MASHARTI NA ADABU ZAKE

Mwandishi

Abu Halima Arafat

## UTANGULIZI WA MWANDISHI

Kila sifa njema anastahiki Allaah. Swala na Salamu zimshukie Nabii wetu Muhammad, Jamaa zake na Maswahaba wake wote.

Baada ya hayo:

Katika Makala yetu iliyopita tumetaja hukumu mbalimbali kuhusiana na mnyama anayefaa kuchinjwa katika Udh-hiya, pia tumeandika Makala nyingine kuhusu Hadithi dhaifu zinazofungamana na Udh-hiya, ili mtu asije akafanya jambo ambalo halijathibiti katika Qur'an na Sunnah, na wala halijafanywa na Salaf Swaalih (wema waliotangulia).

Ndugu muislamu, tunafahamu kwamba kuchinja ni ibada, kwa hiyo lazima itimize masharti yake, ambayo ni Ikhlaas na kumuiga Mtume ﷺ ili ikamilike, na kumnufaisha mfanyaji wake mbele ya Allaah Ta'alaa, wala haifai kuchinja kwa ajili ya mashetani, mizimu n.k.

Kwa ajili hiyo -kwa taufiq ya Allaah- nimeona nikamilishe maudhui hii ya Udh-hiya, kwa kuandika makala nyingine maalumu ikielezea mas'ala ya kuchinja pamoja na masharti yake, kwa sababu huenda mtu akamiliki mnyama ambaye ametimiza vigezo, lakini akawa hajui masharti ya kuchinja wala adabu zake, hatimaye asipate ujira kamili mbele za Allaah wakati wa kuitekelza ibada hii tukufu.

Namuomba Allaah atuonyeshe haki na aturuzuku kuifuata, na atuonyeshe batili na aturuzuku kuiacha.

Wabillaahi Ttaufiiq.

**Abu Halima Arafat Bin Mahmoud**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Maana ya neno **Ad dhabhu** ni: kumwaga damu ya mnyama wa nchi kavu aliye halali, kwa kumchinja, kufanya Nahru au kumjeruhi sehemu yoyote ya mwili wake, kiasi cha kuweza kumtoa damu.

**Nahru ni:** kumtoboa ngamia chini ya shingo (kitobwe) chake, na wakati huo atazingatiwa kisheria kuwa amechinjwa.

**Ama kujeruhi:** hili ni kwa mnyama yoyote ambaye haiwezekani kumkamata na kumchinja kwa njia ya kawaida, sawa awe ni ngamia, ng'ombe, nyati, n.k.

Na ili mnyama huyo awe halali kuliwa lazima yapatikane masharti yafuatayo kwa mchinjaji:

1. Mchinjaji awe ni miongoni mwa watu wenye uwezo wa kukusudia kuchinja, kama vile kuweza kupambanua -linalofaa na lisilofaa-, kuwa na akili timamu n.k, hivyo si halali kuliwa mnyama aliyechinjwa na mtoto mdogo, au mzee sana asiyeweza kupambanua, kadhalika mwenda wazimu na mlevi.
2. Mchinjaji awe ni muislamu -hata kama ni faasiki/muovu-, au awe Ahlul kitaab (anaye jinasibisha na dini ya Uyahudi au Unaswara)[1]. Na mtu anayefanya bidaa ambayo haimtoi katika uislamu, au mtoto mdogo mwenye kupambanua, au mwanamke, ni halali vichinjwa vyao. Amesema Ibnul Mundir - رَحِمَهُ اللهُ -:

**"وَأَجْمَعُوا عَلَى إِبَاحَةِ ذَبِيْحَةِ الصَّبِيِّ، وَالمَرْأَةِ إِذَا أَطَاقَا الذَّبْحَ، وَ أَتَيَا عَلَى مَا يَجِبُ أَنْ يُؤْتَى عَلَيْهِ"**

**"Maulamaa wote wamekubaliana juu ya uhalali wa mnyama aliyechinjwa na mtoto mdogo au mwanamke, ikiwa wataweza kuchinja, na kufanya yote yanayopasa"[2].**

---

[1] - Itafaa ikiwa atalitaja jina la Allaah juu yake, na kama hakulitaja si halali mnyama huyo.

[2] - Tazama kitabu: [Al-ijmaa] (Uk. 75).

Kadhaalika amesema Ibn Qudama - رَحِمَهُ اللهُ - wakati aliponukuu maneno haya katika kitabu chake na kuitaja hadithi ya mjakazi wa Ka'b Ibn Malik -رَضِيَ اللهُ عَنهُ - ambaye alichinja mbuzi kwa jiwe lenye makali na Mtume ﷺ akamkubalia.

«وَفِي هَذَا الحَدِيثِ فَوَائِدُ سَبعٌ؛ أَحَدُهَا، إِبَاحَةُ ذَبِيحَةِ المَرْأَةِ»

**"Katika hadithi hii kuna faida saba: moja yao ni: uhalali wa mnyama aliyechinjwa na mwanamke"(3).(4)**

Amesema Ibn Hazmi - رَحِمَهُ اللهُ -:

«وَلَا أَعْلَم خِلَافًا فِي أَكْلِ مَا ذَبَحَتِ الْمَرْأَةُ الْمُسْلِمَةُ الْعَاقِلَةُ الْبَالِغَةُ عَلَى الشُّرُوطِ الَّتِي ذَكَرْنَا فِي الرَّجُلِ»

**"Wala sijui khilafu yoyote kuhusu uhalali wa kula mnyama aliyechinjwa na mwanamke, muislamu, mwenye akili timamu, baleghe, (akiwa atachinja) kwa kuzingatia masharti yale tuliyoyataja kwa mwanamme''(5).**

Amesema Imam An-Nawawi - رَحِمَهُ اللهُ -:

«وَيَجُوزُ أَنْ يُوَكِّلَ كِتَابِيًّا وَامْرَأَةً وَصَبِيًّا ... وَفِي كَرَاهَةِ تَوْكِيلِ الْمَرْأَةِ الْحَائِضِ وَجْهَانِ (أَصَحُّهُمَا) لَا يُكْرَهُ لِأَنَّهُ لَمْ يَصِحَّ فِيهِ نَهْيٌ»

**"Inafaa kumuweka wakala Ahlul kitaab (Myahudi au Mnaswara), mwanamke na mtoto mdogo ... (kwa ajili ya kuchinja), na kuna kauli mbili kuhusu karaha ya kumweka wakili mwanamke mwenye hedhi (ili akuchinjie), lakini kauli iliyo sahihi zaidi si karaha, kwa sababu halijakuja katika hilo katazo lolote"(6).**

---

3 - Tazama kitabu: [Al-Mughni] (Jz. 9, Uk. 402).

4- Tafauti na Fat-wa aliyoitoa Sheikh Sharifu mwaka ya 2000m akiwa Wete Pemba, kwamba: **[Mwanamke hafai kuchinja kwa sababu ana huruma sana]**. Kauli hii haizingatiwi.

5 - Tazama: [Maraatibul ijmaa] (Uk. 147).

6 - Tazama kitabu: [Al-Majmuu'] (Jz. 8, Uk. 405).

Na huo ndio msimamo wa Jumhuri (maulamaa wengi), amesema Imam Shaukani -رَحِمَهُ الله- wakati akifafanua maneno ya Mtume ﷺ alipo muamrisha Ka'b -رَضِيَ الله عَنه- kula mnyama aliyechinjwa na mjakazi huyo:

«فِيهِ دَلِيلٌ عَلَى أَنَّهَا تَحِلُّ ذَبِيْحَةُ المَرْأَةِ، وَإِلَيْهِ ذَهَبَ الجُمْهُورُ»

**"Katika hadithi hii kuna ushahidi juu ya kwamba mnyama aliyechinjwa na mwanamke ni halali, na huo ndiyo msimamo wa Jumhuri"[7].**

Na Imam Bukhari - رَحِمَهُ الله - ameweka mlango katika sahihi yake unaosema:

«بَابُ ذَبِيحَةِ المَرْأَةِ وَالأَمَةِ»

**"Huu ni mlango kuhusu kichinjwa cha Mjakazi na Mwanamke".**

Kisha akasema Ibn Hajar - رَحِمَهُ الله - :

«كَأَنَّهُ يُشِيْرُ إِلَى الرَّدّ عَلَى مَنْ مَنَعَ ذَلِكَ»

**"Kana kwamba Bukhari anakusudia kumkosoa yule aliyekataza hilo"[8].**

Kadhalika ni halali kula mnyama aliyechinjwa na Ahlul kitaab hata kama wazazi wa mchinjaji huyo si katika Ahlul kitaab.

Ama asiyekuwa katika Ahlul kitaab si halali kichinjwa chake kwa ujumla wa kauli yake Allaah:

﴿وَطَعَامُ ٱلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلْكِتَٰبَ حِلٌّ لَّكُمْ وَطَعَامُكُمْ حِلٌّ لَّهُمْ﴾

**"Na chakula cha waliopewa kitabu ni halali kwenu"[9].**

7- Kitabu: [Nailul Autwaar] (Jz. 8, Uk. 160).
8- Kitabu: [Fat-hul baari] (Jz. 9, Uk. 932).
9- Surat Al-Maida/5.

Amesema Al-Khaazini - رَحِمَهُ اللهُ - katika tafsiri yake:

**« وَأَجْمَعُوا عَلَى تَحْرِيمِ ذَبَائِحِ المَجُوسِ وَسَائِرِ أَهْلِ الشِّرْكِ مِنْ مُشْرِكِي العَرَبِ وَعَبَدَةِ الأَصْنَامِ وَمَنْ لَا كِتَابَ لَهُ»**

**"Wamekubaliana (maulamaa wote wa kiislamu) juu ya uharamu wa vichinjwa vya majusi (waabudia moto) na washrikina wote, katika washirikina wa kiarabu, waabudu masanamu na yule asiyejiegemeza na watu waliopewa kitabu (wapagani)''[10].**

3. Awe amekusudia kuchinja, lau kama alimchinja mnyama bila kukusudia ima kwa kujihami ili mnyama huyo asimdhuru, au alikusudia kukata kitu kingine, tahamaki akamchinja mnyama bila kukusudia, mnyama huyo si halali kuliwa, Allaah amesema:

**﴿إِلَّا مَا ذَكَّيْتُمْ﴾**

**"Ila mkidiriki kumchinja"[11].**

Allaah ameegemeza kitendo cha kuchinja kwa wale anao wazungumzisha, ikafahamisha kwamba anayetaka kufanya jambo hilo lazima atie Nia, kwa sababu mtu atalipwa kwa vile alivyonuwia.

**«إِنَّمَا الأَعْمَالُ بِالنِّيّاتِ، وَإِنَّمَا لِكُلِّ امرِئٍ مَا نَوَى»**

**"Hakika amali zote zinahitaji nia, na hakika kila mtu atalipwa vile alivyonuwia"[12].**

4. Asichinje kwa kumkusudia asiyekuwa Allaah[13], kama kujikurubisha kwa sanamu, mzimu, kaburi, au kuchinja kwa kumtukuza kiongozi, kama vile mfalme, rais au mheshimiwa fulani, na akichinja kwa sababu hizo mnyama huyo si halali kuliwa hata akitamka Bismillaahi, kwa hadithi ya Mtume ﷺ :

---

10- Kitabu: [Tafsiirul Khaazin] (Jz. 2, Uk. 13).

11- Surat al-Maida/3.

12- Bukhari (1). Muslim (155).

13- Kama vile Shetani, Mzimu n.k.

«وَلَعَنَ اللهُ مَنْ ذَبَحَ لِغَيْرِ اللهِ»

**"Allaah amlaani aliyechinja kwa kumkusudia asiyekuwa Allaah"(14).**

5. Asitaje lisilo kuwa jina Allaah, kama vile jina la Nabii (Bismi Nnabiy…), Malaika: (Bisimi Jibril…), au mzimu fulani n.k.

Allaah amesema:

﴿حُرِّمَتۡ عَلَيۡكُمُ ٱلۡمَيۡتَةُ وَٱلدَّمُ وَلَحۡمُ ٱلۡخِنزِيرِ وَمَآ أُهِلَّ لِغَيۡرِ ٱللَّهِ بِهِۦ﴾

**"Mmeharimishiwa nyamafu (mzoga), damu, nyama ya nguruwe na mnyama aliye chinjwa kwa (kutajwa) lisilo kuwa jina la Allaah"(15).**

Amesema Ibn Kathir رَحِمَهُ اللهُ katika kuitafsiri aya hii:

«مَا ذُبِحَ فَذُكِرَ عَلَيْهِ اسْمُ غَيْرِ اللَّهِ، فَهُوَ حَرَامٌ؛ لِأَنَّ اللهَ أَوْجَبَ أَنْ تُذْبَحَ مَخْلُوقَاتُهُ عَلَى اسْمِهِ الْعَظِيمِ، فَمَتَى عُدِلَ بِهَا عَنْ ذَلِكَ وَذُكِرَ عَلَيْهَا اسْمُ غَيْرِهِ مِنْ صَنَمٍ أَوْ طَاغُوتٍ أَوْ وَثَنٍ أَوْ غَيْرِ ذَلِكَ مِنْ سَائِرِ الْمَخْلُوقَاتِ، فَإِنَّهَا حَرَامٌ بِالْإِجْمَاعِ»

**"Mnyama yoyote aliye chinjwa likatajwa juu yake lisilokuwa jina la Allaah, mnyama huyo ni haramu kuliwa, kwa sababu Allaah amewajibisha wachinjwe wanyama wake juu ya kutajwa jina lake tukufu, basi wakati wowote akiepushwa mnyama huyo na hilo na likatajwa juu yake jina la mwingine asiyekuwa yeye Allaah, kama vile jina la sanamu, shetani, mzimu, au viumbe wengine, mnyama huyo ni haramu (kuliwa) kwa makubaliano ya maulamaa wote"(16).**

6. Ataje jina la Allaah juu yake, kwa ajili ya kauli yake Allaah:

﴿فَكُلُواْ مِمَّا ذُكِرَ ٱسۡمُ ٱللَّهِ عَلَيۡهِ إِن كُنتُم بِـَٔايَٰتِهِۦ مُؤۡمِنِينَ﴾

**"Basi kuleni katika walio somewa jina la Allaah juu yake. Mkiwa nyinyi mnaziamini Aya zake"(17).**

---

14 - Muslim (43).

15- Surat Al-Maida/3.

16- Kitabu: [Tafsiri ibn kathir] (Jz.3, Uk. 17).

17 - Suratul An-aam/118.

Na pia amesema:

﴿وَلَا تَأْكُلُوا۟ مِمَّا لَمْ يُذْكَرِ ٱسْمُ ٱللَّهِ عَلَيْهِ وَإِنَّهُۥ لَفِسْقٌ﴾

**"Wala msile katika wale wasio somewa jina la Allaah juu yake. Kwani huo ni upotofu"[18].**

Na Mtume ﷺ amesema:

«مَا أَنْهَرَ الدَّمَ، وَذُكِرَ اسْمُ اللهِ عَلَيْهِ فَكُلُوْهُ»

**"Kitu chochote ambacho kimemwagaga damu[19] na likatajwa juu yake jina la Allaah, basi kuleni"[20].**

a. Sharti ni kwamba atamke jina la Allaah wakati wa kuchinja, wala pasiwepo baina yake kipambanuzi chochote, (mfano) akasema: Bismillaahi, kisha akaenda kunywa maji, halafu akarejea na kumchinja mnyama huyo haitafaa, kwa sababu hiyo ni dua maalumu ambayo sharti lake ni kuwa isomwe wakati wa tukio, na kama ni kipambanuzi kidogo kiasi cha kumlaza mnyama vizuri na kumchinja hapana tatizo.
b. Atamke jina la Allaah kwa mnyama aliyemkusudia kumchinja, akitamka hali ya kuwa amemshika mbuzi, kisha akabadilisha na kumchukua mbuzi mwingine basi atamke upya.
c. Inatakiwa atamke jina la Allaah kwa kusema: **(Bismillaahi)**.
d. Haifai mtu kuacha kwa makusudi kutamka jina la Allaah **(Bismillaahi)**, kwa sababu Mtume ﷺ ameweka sharti kwa mnyama ili awe ni halali kuliwa, kitumike kitu chenye kumwaga damu na litajwe juu yake jina la Allaah, mpaka baadhi ya Maulamaa wanaona kwamba kutamka Bismillaahi wakati wa kuchinja ni sharti, lau mtu aliacha kwa ujinga au kusahau

18 - Suratul An-aam/221.

19 - Anakusudia kitu chochote chenye makali amabcho kinaweza kuchinja na kumwaga damu, Kisu, kigae, jiwe n.k. kinafaa kutumika katika kuchinja.

20 - Bukhari (2488) na Muslim (24).

mnyama huyo si halali kuliwa. Lakini wengine wanaona kuwa ni sunnah, endapo mtu hakutamka bado mnyama huyo ni halali, kwa hiyo muislamu ajitahidi kutamka, wala asiache kwa makusudi, kwa ajili ya tahadhari na kujiondoa kwenye khilafu.

e. Asiikusudie **Bismillaahi** kwa moyo bali aitamke kwa ulimi, na akiwa hawezi kama vile bubu n.k basi atatoa ishara pekee.

7. Achinje kwa kitu chenye makali (chenye kukoa), lakini asitumie kucha wala meno, kwa sababu jino ni mfupa, na haifai kuchinja kwa kutumia mfupa wa aina yoyote, na kucha ni kisu cha Wahabeshi, na baadhi ya Maulamaa wanasema sababu ya kukatazwa kwake:

   a) Itapelekea watu kufuga kucha kwa ajili ya kuzitumia katika kuchinja, na kama inavyojulikana katika sheria ya kiislamu kwamba haifai mtu kufuga kucha zake kwa kuzirefusha.
   b) Kuchinja kwa kutumia kucha ni kujifananisha na ndege au wanyama wakali wenye kushambulia, ambao sisi tumefadhilishwa juu yao na tumekatazwa kujifananisha nao.

8. Kuhakikisha kwamba anamwaga damu, na hilo lina hali mbili:
   a) Endapo mnyama imeshindikana kumkamata, ima kwa kuwa amekimbia au ametumbukia kisimani, kiasi ambacho haiwezekani kumpata na kumchinja kwa njia ya kawaida, katika hali hii atapigwa katika sehemu yoyote ya mwili wake mpaka afe, na iliyo bora itumike zana ambayo itaweza kumtoboa na kumuua kwa haraka, wala lisitumike mfano wa rungu au fimbo n.k, kwa sababu haviwezi kumtoboa na kumwaga damu.
   b) Ama akiwa ni mnyama ambaye anaweza kudirikiwa na kukamatwa, ni sharti achinjwe katika shingo yake kwa kukata mshipa mkubwa wa pumzi, chakula na kinywaji, na mishipa miwili minene iliyozunguka mshipa wa pumzi na mshipa wa chakula na kinywaji.

9. Awe mchinjaji ameruhusiwa kisheria, na kutoruhusiwa kisheria kuna hali mbili:
   a) Ni kuwa amezuiwa kuchinja kwa ajili ya haki ya Allaah, kama alivyozuiwa mtu aliyehirimia Hija au Umra kuwinda, ikiwa atawinda mnyama na akamchinja, mnyama huyo ni haramu kuliwa, kadhaalika akiwinda mtu mwingine kisha akampatia yeye ili amchinje, au yeye ndiye alimuashiria mtu mwingine (ambaye hajahirimia) mnyama wa kuwinda, Allaah anasema:

﴿وَحُرِّمَ عَلَيۡكُمۡ صَيۡدُ ٱلۡبَرِّ مَا دُمۡتُمۡ حُرُمٗاۗ﴾

**"Na mmeharimishiwa kuwinda wanyama wa bara muda wa kuwa mmehirimia"[21].**

   b) Au amezuiwa kwa ajili ya haki ya mwanadamu, mfano kumchinja mnyama ambaye hammiliki, wala hajaruhusiwa na mwenyewe, au mnyama wa wizi n.k. ni haramu kula mnyama huyo kwa mchinjaji na kila anayejua kuwa ni mnyama wa wizi.

**Adabu za kuchinja:**

Kama ilivyokuwa kuchinja kuna masharti ambayo huzingatiwa pia kuna adabu ambazo inapasa kuzijua, miongoni mwa hizo:

1. Mnyama kumuelekeza upande wa kibla.
2. Kumtendea wema, kwa kutumia kifaa chenye makali.
3. Kupitisha mkono wake kwa nguvu shingoni kwa mnyama.
4. Ngamia huchinjwa akiwa amesimama kwa miguu mitatu, hali ya kuwa umenyanyuliwa juu na kufungwa mguu wake (wa kushoto), na anatobolewa chini ya kitobwe cha shingo yake.
5. Asiyekuwa ngamia huchinjwa hali ya kuwa amelazwa kwa ubavu wake wa kushoto, na mchinjaji ataweka mguu wake juu ya shingo yake, ama anayetumia mkono wa kushoto basi atamlaza kwa ubavu wa kulia, kisha atashika kichwa chake na

[21] - Suratul Maida/96.

kukinyanyua kidogo ili aone vizuri mahala pa kuchinja, wala asimzuie mnyama mikono na miguu yake wakati wa kumchinja, na ikipelekea kufanya hivyo basi iwe kwa upole ili aweze kujitikisa na kutoa damu kwa wingi.

6. Mchinjaji akamilishe kukata mshipa wa pumzi, mshipa unaopita chakula na kinywaji, na mishipa miwili migumu iliyo pembezoni mwake.
7. Asitoe kisu chake isipokuwa wakati wa kutaka kuchinja.
8. Kuleta takbira baada ya kutaja jina la Allaah wakati wa kuchinja: **(Bismillaahi, wallaahu akbar)**.
9. Kutaja jina la mwenye mnyama huyo wakati wa kuchinja Udh-hiya au 'Aqiiqa, lakini kama atakusudia tu kwa moyo itatosha.
10. Kuomba dua baada ya kumaliza kuchinja:

**«بِاسْمِ اللهِ، اللهُمَّ تَقَبَّلْ مِنْ مُحَمَّدٍ، وَآلِ مُحَمَّدٍ، وَمِنْ أُمَّةِ مُحَمَّدٍ»**

**"Bismillaahi, ewe Allaah mkubalie Muhammad, na Jamaa wa Muhammad, na watu wote wa umati wa Muhammad". [Muslim] (19).**

### Mambo ya karaha wakati wa kuchinja

1. Kuchinja kwa kutumia kifaa kisicho na makali.
2. Kumchinja mnyama mmoja hali ya kuwa mwenzie anatazama.
3. Kumfanyia mambo ya karaha kabla ya kumchinja, kama vile kumvunja kiungo chake, bali kufanya hivyo ni haramu, au kumtolea maneno yasiyofaa; leo ndio mwisho wako, n.k.
4. Kunoa kisu chako hali ya kuwa mnyama anakiona.

Wallaahu A'lam.

Namuomba Allaah aturuzuku Ikhlaas katika kauli na amali zetu.

Usiku wa Ijumaa 10/Dhul-hijja/1446^H – 6/6/2025^M
Tanzania.
Simu: 0715263253.